

## Maswali

1. Eleza kwa maneno yako vile Ufalme utakuwa?
2. Chora picha uonyesha vile Ufalme utakuwa?
3. Unatazamia nini kwa Ufalme?
4. Tunaweza kuwa kwa ufalme baada ya nini?
5. Ufalme wa Mungu utakuwa lini?
6. Utakuwa wapi?
7. Mji gani ndio utakuwa mji mkuu?

## Majibu

4. Baada ya kuamini, kutubu na kubatizwa.
5. Yesu atakaporudi hapa duniani.
6. Hapa duniani.
7. Yerusalemu.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 30 Unabii wa Ufalme

## Marejeo

Isaya 35

## Kiini cha somo

Kufikiria juu ya ufalme wa Mungu utakaokuja hapa duniani.


## Maneno maalum

1. Yerusalemu + Yesu + dunia yote.
2. Mtawala mzuri + uamuzi mwema + haribu uovu.
3. Hakuna jangwa + nafaka +simba na nyoka.
4. Vita + vifaa.
5. Kipofu + kiziwi + kiwete + bubu.
6. Hakuna kifo + Mungu + yakale kwisha.
7. Soma + Amini + Batizwa + ishi maisha mazuri.

**30.1** Isaya 2:3, Zekaria 14:9: Katika ufalme, kutakuwa na Mfalme, kutakuwa na mji mkuu na kutakuwa na pahali Mfalme atatawalia. Kwa Ufalme wa Mungu, Yesu atakuwa mfalme atakaporudi hapa duniani. Isaya 2 anatwambia sheria zote zitatoka Yerusalemu kwa hivyo Yerusalemu itakuwa mji mkuu. Zekaria 14:9 anatwambia kwamba Yesu atakuwa Mfalme kwa dunia yote. Watu wote wataabudu Mungu na wataenda Yerusalemu kusherehekea sikukuu sote.


**30.2** Isaya 11:1-5: Tunaambiwa kwamba Yesu atakuwa mtawala mzuri. Hatakuwa kama watawala wa saa hii wabaya na wafisadi. Atakuwa haki. Atakuwa na nguvu za Mungu na kujua la kufanya na vile anaamua maneno vizuri. Hatakuwa mfidadi. Atasaidia watu maskini na ataharibu waovu.

**30.3** Isaya 35:1, 2. Kwa ufalme, dunia yote itabadilika. Dunia itakuwa vile ilikuwa katika Bustani ya Edeni. Isaya anatwambia kwamba hakutakuwa na jangwa- nchi itakuwa yenye rutuba tele. Kutakuwa na mito kwenye kuna jangwa sasa. Zaburi 72 inatwambia kutakuwa na nafaka juu ya milima. Juu ya milima kuna baridi sana na nafaka haiwezi kukuswa huko, lakini kwa huo ufalme itakuwa tu vyema. Wanyama watakuwa wazuri na hawatapigana na kuuana. Watoto watacheza na simba na nyoka.



**30.4** Mika 4:3: Hakutakuwa na vita au kupigana kwa ufalme wa Mungu. Watu hawatazungumza juu ya vita tena. Silaha zote zinazotumiwa vitani zitategenezwa ili ziwe vifaa vya kufanya kazi nchini. Kila watu watakuwa na chakula chao na kukaa kwa amani.

**30.5** Isaya 35:5, 6. Hakutakuwa na ugonjwa katika ufalme huo. Hakutakuwa na watu vipofu, watu viziwi, watu wasiotembea vizuri au, watu wasiozumngumza vizuri kwa huo ufalme. Mungu ataondoa magonjwa yote.



**30.6** Ufunuo 21:4: Vizuri zaidi. Mwishowe Mungu akiwa mfalme, hakutakuwa na kifo. Hakutakuwa na maombolezo, au machozi, kwa sababu Mungu atapanguza kila mtu machozi. Yakale yote yatakwisha.

**30.7** Marko 16:16: Unapenda kuwa kwa huu Ufalme? Inaonekana ni pahali pazuri. Mungu amesema kwamba kila mtu mme au mke anaweza kuwa huko, akitaka. Lakini lazima tufanye kitu kwanza. Tunatakiwa tusome Biblia na tumjue Mungu. Lazima tumwamini na kuomba msamaha kwa dhambi zetu zote. Tubatizwe katika Yesu. Tujaribu kuishi maisha mazuri tukiiga mfana wa Yesu mpaka atakaporudi. Tukifanya haya yote, Mungu ataturuhusu tuwe kwa Ufalme wake.